JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

**HOTUBA YA MHE. DKT. DAMAS DANIEL NDUMBARO (MB), WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA WAKATI WA KUMKARIBISHA MHE. RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. SAMIA SULUHU HASSAN KWENYE MKUTANO MKUU WA MAWAKILI WA SERIKALI KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA JAKAYA KIKWETE CONVENTION CENTER DODOMA, TAREHE 29 SEPTEMBA, 2022.**

Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Mhe. Prof. Ibrahimu Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania;

Mhe. Dkt. Tulia Akson (MB), Spika wa Bunge, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Mhe.Jenista Mhagama (MB), Waziri Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora;

Mhe.Innocent Bashungwa (MB), Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

Mhe. Jaji Dkt.Elizer Mbuki Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

Mhe.Dkt. Mwinyi Tali Haji, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;

Bi. Mary Gasper Makondo, Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria,

Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Mhe. Dkt. Evaristo Longopa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali,

Dkt. Khatibu Kazungu, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria;

Prof.Edward Hosea, Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika,

Waheshimiwa Wanasheria Wakuu wastaafu,

Waheshimiwa Majaji Wastaafu,

Wakuu wa Idara na Taasisi za Serikali Mliopo;

Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria,

Mawakili wa Serikali Mliopo;

**Waandishi wa habari;**

**Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana.**

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kazi Iendelee.***

Napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutukutanisha hapa siku ya leo katika Mkutano huu wa Mawakili, ambao ni Mkutano wa Pili baada ya mkutano wa kwanza kufanyika tarehe 30 hadi 31 Agosti, 2018 ukiwakutanisha mawakili wote wa Serikali. Mkutano wa mwaka huu unaongozwa na Kauli Mbiu isemayo, ***"Utekelezaji wa Majukumu Unaozingatia Sheria ni Nyenzo Muhimu kwa Maendeleo ya Taifa.***

***Mheshimiwa Rais,*** Kipekee napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kukubali mwaliko na kutenga muda wako na kushiriki pamoja nasi katika mkutano huu muhimu pamoja na majukumu mengi uliyo nayo. Tunasema karibu sana Mhe. Rais.

***Mheshimiwa Rais,*** Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshmiwa Mawaziri Mliopo na Waheshimiwa Wabunge mliopo napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru na kuwakaribisha wawezeshaji, mawakiili wa serikali, watumishi wote na wageni wote waliofika kushiriki nasi katika mkutano huu tunasema karibuni sana.

***Mheshimiwa Rais,***

Mkutano huu wa Mawakili wa Serikali umejumuisha Mawakili kutoka Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa maana ya Wizara, Idara na Wakala za Serikali. Kwa kutambua kuwa mawakili wa serikali wengi wapo chini ya usimamizi wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yaani Ofisi ya Rais TAMISEMI, ndio maana tumeona ni vyema pia na Mhe.

Innocent Bashungwa (Mb), Waziri kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI akashiriki nasi katika mkutano huu ili iwapo kuna maelekezo yoyote kutoka kwako Mhe. Rais au kuna masuala ya kisheria yatakayohitaji utekelezaji yaweze kufanyiwa kazi kwa uharaka.

***Mheshimiwa. Rais,***

Mkutano huu wa Mawakili wa Serikali ni Mkutano muhimu ambao utakwenda kuleta tija kwa mawakili wa serikali ambao ndio watekelezaji wa majukumu mbalimbali kuhusiana na masuala yote ya kisheria na utoaji haki nchini hususan kwenye masuala yahusu uandaaji wa Mikataba, uandaaji wa nyaraka mbalimbali za mahakama, uendeshaji wa mashauri mahakamani na utiaji saini wa mikataba mbalimbali yenye tija kwa nchi yetu n.k.

***Mheshimiwa Rais,***

Mkutano huu ambao ulitanguliwa na mkutano uliofanyika siku ya jana tarehe 28 Septemba, 2022 uliohusisha Wakuu wa Idara na Vitengo vya Sheria kutoka Wizara, Idara na Wakala za Serikali kutoka Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, utajadili masuala mbalimbali kuhusiana na Chama cha mawakili wa serikali, maadili yao n.k. yatajadiliwa na kuwekewa maazimio ya kuboresha na kuifanya taaluma ya sheria katika utumishi wa Umma iweze kusonga mbele kwa ufanisi.

***Mheshimiwa Rais,***

Mkutano huu pia utajadili masuala ya kiutumishi yanayowagusa mawakili wa serikali kwa ujumla wake ndio maana tunaye Mhe.Jenista Mhagama (Mb), Waziri Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ili kama kuna

masuala au maelekezo kutoka kwako yatakayohitaji utekelezaji yafanyiwe kazi haraka iwezekanavyo.

***Mheshimiwa Rais,***

Mawakili wa Serikali wameunda chama chao ambacho kitakuwa ni kiunganishi baina yao katika kuwekeana mipango na mikakati itakayosaidia kuboresha taaluma ya sheria na kusimamia maadili baina yao. Sambamba na hilo, chama hiki kinachoitwa Public Bar Association au Chama cha Mawakili wa Serikali kilichoanzishwa kwa TS Na.589 ya mwaka 2019 ambapo ukiridhia tutaomba utuzindulie leo Mhe. Rais ili kianze kufanya kazi rasmi na kesho tunaimani viongozi wa chama hiki watapatikana kwa njia ya kuteuliwa kama miongozo ya kusimamia chama hiki inavyofafanua.

***Mheshimiwa Rais,***

Kupitia Chama cha Mawakili wa Serikali, tunatarajia kuwa na umoja wenye nguvu na kuwa jukwaa la kuishauri Serikali katika masuala mbalimbali yakiwemo maslahi yao, pasipo kuingiza harakati na siasa, kikijikita katika madhumuni ya kuanzishwa kwake yakiwemo:

a) Kuwa jukwaa la majadiliano la masuala mbalimbali;
b) Kuwakilisha mawazo ya wanachama yanayoathiri taaluma yao;
c) Kuimarisha mfumo wa kisheria inayoathiri sekta ya sheria katika Utumishi wa Umma; na
d) Kusimamia na kuendesha mafunzo mbalimbali kwa mawakili walio katika utumishi wa Umma;

***Mheshimiwa Rais,***

Kwa kuwa siku hii ni yako, na ninatambua wewe kama Mama na kama tujuavyo, mama siku zote furaha yake ni kuona watoto wake wakikaa kwa

upendo na kwa umoja, na watoto siku zote huwa ni wasikivu pale mama anapozungumza au kutoa maagizo, Kwa mara nyingine, kwa niaba ya Wizara, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mawakili wa Serikali wote naomba tena nikushukuru sana kwa kukubali wito wetu na kujumuika nasi siku ya leo. Sasa naomba nikukaribishe uweze kuongea na mawakili wa Serikali ambao wapo tayari kukusikiliza kwa sasa.

***Mungu Ibariki Afrika***

***Mungu Ibariki Tanzania,***

***Asanteni sana kwa kunisikiliza.***